# TUMCHAO BWANA NDIYO WAKATI WETU KUSEMA SASA
# MAANDIKO: ZAB. 118: 1 – 4, 5-29

1. **UTANGULUZI**
   Wakati wana wa dunia wakiwa na misemo yao, tumchao Bwana nasi lazima tuwe na misemo yetu, wakati wana wa dunia hii wakiwa na nyimbo zao na aina ya mitindo yao ya kuimba na aina ya mitindo yao ya kushona ya kuvaa; na aina ya mitindo yao ya kucheza; tumchao Bwana tuwe na mitindo ya kuimba nyimbo zetu; tuwe na aina tofauti kabisa ya mitindo yetu ya kuvaa; tuwe na aina tofauti kabisa ya kucheza kwetu mbele za Mungu wetu pamoja na jinsi ya kumwabudu.

- Kanisa leo lina madai kama haya, wanataka waenende kama mataifa wanavyoenenda. ***1Samwl. 8: 4 – 9.***

- Inasemekana kwamba kabla ya Yesu kwenda katika bustani ya Gethsemani na wanafunzi wake kuomba mara ya mwisho kabla ya kukamatwa na kwenda kusulubiwa msalabani aliimba na wanafaunzi wake(Mitume) Zaburi **hii ya 118;** na Yesu atakapokuwa anarudi mara ya pili pamoja na mwaliko akiongozwa na Malaika Mkuu na parapanda ikipigwa; wimbo utakaokuwa ukiimbwa utakuwa ni Zaburi hii***!! Math. 26:29-30*** (***Mark. 14:26)*** halafu soma vema ***Zab. 118:26*** na ***Math. 23:37-39!!***

2. Zaburi hii ya **118** kwanza iliimbwa na Mfalme Daudi alipokuwa anaingia Hekaluni ili kumtolea Mungu dhabihu za shukrani baada ya kuwashinda mataifa makubwa waliokuwa na nguvu kuliko Taifa la Israeli na akapokewa na makuhani waliokuwemo hekaluni wakihudumu pamoja watakatifu waliokuwa wamekutanika na akawasimulia aliyoyatenda Bwana kwa mkono wake hodari na akawasihi wamshukuru Mungu kwa kuwaokoa Israel kwa neema ya ajabu; ndiyo sababu hata Yesu

aliimba Zaburi hii wakati alipokuwa anaenda kukamilisha wokovu mkuu na wa ajabu kwa wanadamu ambao shetani alishawateka na kujitangaza kama bwana wao na kuwatumikisha kwa mateso na magonjwa kama alivyokuwa anataka. Kama shetani angefahamu ushindi unaokwenda kutokea baada ya Yesu kuteswa na kisha kufufuka siku ya tatu; asingemsulubisha kabisa Yesu. Daudi asingeona mwisho wa waovu asingestuka kabisa. ***Zab. 73: 1 - 19***

- **Unajua**; ukisoma **Zaburi ya 105, 106** na **118** utakuta zote ni kama zinafanana maadamu zinanukuu matendo makuu aliyoyatenda Bwana kwa mkono wake hodari kwa Taifa la Israel katika ***1Nyak. 16:1-36***
- Ndiyo sababu Mfalme Daudi hakutaka kabisa wana wa Israel wakati wa utawala wake wasahau kumshukuru Mungu kutokana na matendo yake makuu na ya ajabu kwa Taifa la Israel; na Zaburi za kumshukuru Mungu nyingi ziliandikwa na Mfalme Daudi- ***Zab. 105:1-45***

3. **<u>Siri kuu tatu alizokuwa nazo Mfalme Daudi katika maisha yake ndani ya moyo wake kuhusu Mungu wake ni hizi:-</u>**

*a.* ***Zab. 118:5-9*- Mfalme Daudi alimwona Mungu kuwa ndiye kimbilio lake na salama pekee wakati wote wa maisha yake. (The Lord is my REFUGE);** yeye Mfalme Daudi alipokabiliana na mambo magumu alimkimbilia Bwana maana alifahamu fika kwamba Bwana ndiye salama yake pekee. ***1Saml. 30:6-8, 2Samwl. 2:1-7, 2Samwl. 5:17-21;*** Hili ni fundisho kuu kwa watoto wa Munguleo; tusikimbilie watu kama salama yetu saa ya mambo magumu; tumkimbilie Bwana na tumtwike yeye fadhaa zetu zote maadamu uwezo wa kuzitatua anao. ***Math. 11:28-30. Soma Zab. 118: 7 -9***

b. **Siri ya pili ya ajabu sana na ya pekee aliyokuwa nayo Mfalme Daudi ndani ya moyo wake kuhusu Mungu ni ile ya kufahamu**

**kwamba Bwana pekee ndiye msaada wake hata kama anakutana na mambo magumu na mazito‼!** ***Zab. 118:13,*** **Zab.56:10, Zab. 12-13- (The Lord is my Helper)** ***Zab. 118:10-13), 2Wafalm. 6:15-17*****, 2Nyakat. 16: 7 – 9, 2Nyakat. 32: 7 – 8.**

- Mfalme Daudi wakati alipokuwa anakabiliana na mambo magumu na hasa majeshi ya maadui ambao lengo lao lilikuwa ni kuifuta kabisa. Israel katika uso wa duniani, Hata pale alipohisi kwamba adui wamemzingira kama nyuki; yeye Mfalme Daudi ndani ya moyo wake hakuogopa maana alikuwa anafahamu jinsi Mungu alivyomzingira na kwamba baada ya muda adui hawa hawatakuwa kitu tena na atawakatalia mbali wote kwa msaada wa Bwana. Nasi tukifunguliwa macho ya rohoni katika hili; hatutayumbishwa tena na shetani anayeunguruma kama simba ili kutuogopesha. ***1Petr.5:8- sikia anavyokiri mwanaume – Zab. 118: 10 – 12.***

c. **Siri ya tatu kabambe aliyokuwa nayo moyoni; mwake Mfalme Daudi "THE LORD IS MY SALVATION" yaani Bwana ndiye mwokozi wake, ndiye mtetezi wake, ndiye anayepigana vita vyake vyote. Zab. 118:14-17, 21**

   **Note: Zaburi kama hii aliimba Mtumishi wa Mungu Musa pamoja na wana wa Israel baada ya Bwana kuwaokoa na mkono wa Farao na kuwavusha kwa maajabu yake makubwa katikati ya bahari ya Shamu. Kut. 15:1-20.**

4. **Leo nataka niwaambie wacha Mungu wazi kuwa, wakati wana wa Dunia wanakuwa na misemo yao na nyimbo zao; sisi lazima tuwe na misemo yetu pamoja na nyimbo zetu kama Musa na kama Mfalme Daudi. Bwana aliyewakatilia mbali adui zetu mwaka jana hajabadilika; hata sasa yuko kazini‼**

- Kama Musa alivyoimba wimbo wa ushindi na watu wake baada ya Bwana kuwaokoa na mkono wa Farao, nasi lazima tuimbe daima matendo makuu ambayo Mungu ametutendea; nasi Yesu Kristo ametuokoa kwa jinsi ya ajabu sana na dunia hii ambayo imemeza watu wakuu na matajiri na wasomi; tunalindwa na

majeshi yake **na hakika Yesu Kristo ameongeza thamani ya maisha yetu; watu wanatushangaa kwamba tunaishi bila hirizi tunafanya biashara bila kwenda kwa waganga wa kienyeji? Hii ni ajabu kwa ibilisi japo sisi tunaona kama jambo dogo na la kawaida!!!**

5. **Ngoja nimalizie kwa kueleza Zab. 118:15-17.**
   **Mara tatu Mfalme Daudi anasema juu ya mkono wa Kuume wa Bwana umetenda Makuu, na hata Nabii Isya akasema – Isay.41:10, na hata Yesu Kristo mwenyewe baada ya kufufuka ameketi mkono wa Kuume wa Mungu Baba – Math.26:64, Mar.14:64, 16:19, Mdo. 2:33, Mdo.7:55-56, Rum.8:34, Ebr.1:3, Ebr.10:12, 12:2, 1Petr.3:22 na Ufun. 5:1-14.**

   **Mkono wa Kuume wa Bwana (denote) unamaanisha nguvu/uweza alionao Mungu tayari kumchakaza kabisa shetani na kuwabariki watu wake wamchao!!**
   Sisi ni watu wa thamani sana machoni pa Mungu wetu; ndiyo sababu hatufi vifo vya hovyo hovyo bali vile ambavyo ni makusudi yake Mungu; na hakuna silaha itakayoinuka juu yetu ambayo itafanikiwa!! ***Isay. 54:17***

   Unajua, zamani mataifa makubwa na yenye nguvu yalikuwa yanashirikiana (yanaungana (alliance) na mataifa madogo pale yalipokuwa yanaona kwamba yananufaika/yanafaidika na muungano huo, vinginevyo kama yaliona mataifa hayo madogo kwamba hayana chochote cha thamani cha wao kunufaika kwacho walikuwa wanaangamiza kabisa Taifa hilo; na Israel ndivyo ilivyoonekana mbele ya mataifa makubwa yanayoizunguka kwamba haifai kuwepo katika orodha ya mataifa duniani zaidi ya kuangamizwa ; mkono wa kuume wa Mungu Baba wenye nguvu na uweza wote ukaitwaa **Israel (the rejected stone (Zab. 118:22) and made Israel the capstone of his own kingdom on this earth akafanya Israel**

**iliyodharauliwa kuwa nchi ya thamani na ya pekee duniani hadi sasa; ndiyo sababu** hadi leo katika Israel wakati wa Pasaka lazima waimbe Zaburi hii kwa kukumbuka mkono wa kuume wa Bwana uliowatoa Misri ambapo Farao alipanga kuwaangamiza wote na badala yake akaangamizwa yeye na majeshi yake. ***Math. 21:8-11 ( Zab. 118:25-26.)***

**Note: Unapookoka unapoteza faida (ushirika) na shetani, na mkakati wake ni kukuangamiza tu; anashindwa kutuangamiza kwa sababu ya mkono wa Bwana Yesu ulio juu yetu kama ambavyo alishindwa kumwangamiza Petro kabla ya wakati wake kufika. Mdo. 12:1, Mdo.5:17-21, Mdo. 16:19-34.**

Na unaposoma ***Math.21:9, 23:39, Mark.11:9, Luk.13:35*** na ***Yoh.12:13-*** Haya ni maneno yaliyonukuliwa kutoka **Zab.118: 25-26** yote yakiwa na lengo la kumshukuru pamoja na kumtukuza Bwana Yesu Mwokozi. Mfalme Daudi anamalizia Zaburi yake kwa kushukuru akisema ***"Zab.118:28-29;*** ndiwe Mungu wangu nami nitakushukuru, ndiwe Mungu wangu nami nitakutukuza!! shetani alitaka siku nyingi atufute juu ya uso wa nchi baada tu ya sisi kuokoka; Bwana Yesu amekuwa salama na ngome yetu; shetani aliweka vikwazo na hila nyingi ili tuangamie lakini Bwana ametusaidia kuviruka; shetani alichimba mashamo mengi ili tutumbukie na kuangamia kabisa lakini Bwana Yesu ametutetea na kutuokoa!! Yesu wewe ndiye Mungu wangu na ngome yangu-Nitakushukuru na kukutukuza daima. **Amina.**

***Na***
***Askofu Dr.L.M. Mwizarubi.***
***Dec. 2021***